Habarileo Jumanne Mei 26, 2026 Pg 5

# Madereva daladala Arusha wakubali kusitisha mgomo

**Veronica Mheta na Yasinta Amos, Arusha**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na uongozi wa madereva wa daladala jijini Arusha wamekubaliana kurejesha huduma ya usafirishaji wa abiria kuanzia jana mchana.

Latra ilifanya makubaliano hayo baada ya madereva wa daladala kugoma kutoa huduma kwa takribani saa saba.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Arusha, Amani Mwakalebela alilieleza HabariLEO kuwa baada ya kikao kati ya madereva na Latra, madereva hao walikubali kusitisha mgomo na kuahidi kuendelea kutoa huduma kwa kutoza nauli ya Sh 700 badala ya Sh 1,000 kwa kituo ambacho abiria atashuka.

"Tumekaa kikao na madereva na wamekubali kutoza nauli ya Shilingi 700 badala ya Shilingi 1,000 waliyokuwa wanatoza awali na wameahidi mchana wa jana kuendelea kutoa huduma kama kawaida, na sisi tunafuatilia kuona kama watatoa huduma kama walivyoahidi au la ili tuchukue hatua zaidi," alisema Mwakalebela.

Alisisitiza kuwa nauli ni Sh 700 kutoka kituo hadi kituo na si Sh 1,000. Alisema kama kuna umbali kidogo nauli haipaswi kuzidi Sh 1,500.

Maeneo ambayo yaliathirika na mgomo huo wa daladala ni pamoja na Ngaramtoni kwenda Stendi Ndogo, Kwamorombo, Uswahili Dampo, Ngusero na Majengo.

Bajaji zilizokuwa zikitoa huduma kwenye baadhi ya maeneo zilikuwa zikisimamishwa na wapigadebe na kushusha abiria kwa madai wakubali kuunga mkono mgomo huo.

Aidha, baadhi ya madereva wa daladala wanaofanya safari zao kuanzia Kituo cha Stendi ndogo ambao hawakutaka majina yao yaandikwe katika gazeti, walisema waliamua kusitisha huduma ya usafirishaji wa abiria kutokana na changamoto ya nauli.

"Sisi tuliongea na abiria wetu wanaosafiri kuanzia hapa Stendi Ndogo kwenda Ngulelo, Tengeru hadi Kikatiti kwamba kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta, tunaomba nauli iwe Shilingi 1,000 kutoka kituo hadi kituo, wakakubali," alisema mmoja wa madereva hao.

Alisema nauli hiyo ya Sh 1,000 kutoka Stendi Ndogo inaishia Tengeru wakati ya Usa River Sh 1,500, Maji ya Chai Sh 1,500 na Kikatiti Sh 2,000.

"Changamoto iliyotukuta ni kwamba Latra wanakuja barabarani na kuuliza abiria wametozwa Shilingi ngapi, na abiria wanasema tumetozwa Shilingi 1,000; kisha wanatuuliza sisi, nauli tuliyopanga ni Shilingi ngapi?" alieleza.

Aliendelea, "… tunawaambia kuwa tumeongeza Shilingi 100 kwenye nauli ya awali kituo hadi kituo kwa kuwa nauli ya kwanza ilikuwa kituo hadi kituo Shilingi 600, lakini wameongeza Shilingi 100 pale kwenye Shilingi 600 inakuwa Shilingi 700, kwenye Shilingi 700 ni Shilingi 800 na kwenye Shilingi 900 ni Shilingi 1,000."

Kwa mujibu wa madereva, kulingana na nauli ambayo wamepangiwa na Latra, wakijaza abiria hadi Kikatiti wanapata kati ya Sh 30,000 na 35,000.

"Ukienda na kurudi, unapata Shilingi 60,000 au hata 70,000 wakati gharama ya mafuta unayoweka kutoka Stendi Ndogo hadi Kikatiti kwenda na kurudi unatumia kati ya Shilingi 65,000 hadi 70,000," alisema mmoja wa madereva.

Kutokana na hilo, waliiomba LATRA kuangalia upya bei hizo elekezi ili kuendana na hali halisi ya bei za mafuta.